

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



08 FEBRUARI, 2021



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

KIKAO CHA TANO – TAREHE 08 FEBRUARI, 2021

I. DUA:

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi:

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

### **IV. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **58. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatengeneza eneo la Katokoro linalounganisha Kata za Katoro na Kyamulaile katika Jimbo la Bukoba Vijiji ili kuondoa adha ya usafiri inayowakabili Wananchi wa maeneo hayo.

##### **59. MHESHIMIWA YAHAYA OMAR MASARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi ya Mhe. Rais ya ujenzi wa barabara ya Km 10 katika Mji wa Itigi utaanza.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **60. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kumekuwa na ongezeko la Wanyama Pori katika Hifadhi ya Selous na sasa Tembo na Nyati wanavamia mashamba pamoja na makazi ya Wanakijiji na kuleta tataruki:-

Je, Serikali inaweza kuwarudisha Wanyama hao porini mbali zaidi na Wananchi.

### **61. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itarudia zoezi la kuweka alama za mipaka kwa kuwashirikisha Wananchi ili kumaliza mgogoro uliopo wa mipaka kati ya Hifadhi ya Kitulo na Wananchi wa Vijiji vya Misiwa, Makwalanga, Igofi na Mkondo.

**62. MHESHIMIWA SILLO DANIEL BARAN  
(BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itamaliza migogoro ya mipaka kati ya Hifadhi ya Tarangire na Vijiji vya Gijedabung, Ayamango, Gedamar na Mwada katika Jimbo la Babati Vijijini.

**63. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO  
(ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Serikali imeongeza viwango vya Tozo za Utalii kwa Hifadhi zilizo chini ya TANAPA kuanzia mwezi Julai 2021:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kusitisha Tozo hizo ili kutoa fursa kwa Sekta ya Utalii nchini ambayo imeathirika sana na ugonjwa wa Corona.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**64. MHESHIMIWA HUSNA JUMA SEKIBOKO  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutoa fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa Wakuu wa Polisi wa Wilaya kama inavyotoa kwa Wakuu wa Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.

**65. MHESHIMIWA JACKLINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali imeweka mpango gani wa elimu ya Sheria ya usalama barabarani kwa Madereva wa bodaboda ili waendeshe kwa kutii Sheria na kuepusha kusababisha ajali.

**66. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi ya kukabidhi kwa Wananchi wa Vijiji vya Msanda Muungano, Songambele na Sikaungu shamba lililokuwa limechukuliwa na Jeshi la Magereza Molo Sumbawanga, lenye ukubwa wa hekari 495.

## **WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

### **67. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itaongeza bajeti ya kuboresha elimu katika Vyuo vya Ufundı VETA Mkoani Manyara ili kuboresha utoaji elimu ya ufundi.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **68. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA (CHUNYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini ujenzi wa mradi mkubwa wa maji Chunya Mjini na Kata za jirani utaanza kutekelezwa.

### **69. MHESHIMIWA LEMBULIS SAPUTI MOLLEL (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha usambazaji wa maji kwenye Vijiji vya Engutukoiti, Losinani Juu, Losineni Kati, Oldonyawasi, Lemanda, Lemengrass, Oldenyosambu, Likurat,

Olkeejulbendet, Lenigjape, Olkokula, Lemanyata Lenjani, Seuri, Ekenywa na Ngaramtoni na Kata za Kimyak, Sambasha Tarakwa, Oloirien, Kiranyi, Likidingla, Sokon II, Olturito, Bangata, Mlanganini, Nduruma, Bwawani, Oljoro na Lahni Musa, Kisango, Mwandet Wilayani Arumeru.

**70. MHESHIMIWA SIMON SONGE LUSENGEKILE (BUSEGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini mradi wa maji wa Nyashimo, Kata ya Nyashimo ambao ulitegemewa kukamilika mwezi Oktoba, 2020 utakamilika ili Wananchi waweze kupata maji safi na salama.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**71. MHESHIMIWA AMANDUS JULIUS CHINGUILE (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Masasi – Nachingwea kwa kiwango cha lami utaanza.

## **72. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kuanzia njia panda ya Kongwa hadi Mpwapwa Mjini yenyeye urefu wa takribani Km. 30 ambayo ipo katika llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 – 2025.

### **V. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendelekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) na Mapendelekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/22 pamoja na Mapendelekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22.

**DODOMA**  
**08 FEBRUARI, 2021**

**S. KAGAIGAI**  
**KATIBU WA BUNGE**